



**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU
TANZANIA**



TAAARIFA KWA UMMA

UZINGATIAJI WA SHERIA NA MATUMIZI YA VIBALI KATIKA UINGIZAJI NA USAFIRISHAJI WA MIMEA, MAZAO NA VIUATILIFU NCHINI

Arusha, 28 Septemba, 2026

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) inapenda kuwakumbusha na kuwasisitiza Waagizaji, Wasafirishaji, Wakulima, Mawakala wa Forodha pamoja na Wadau wote wa biashara ya mimea, mazao na Viuatilifu nchini kuzingatia kikamilifu Sheria ya Afya ya Mimea (Sura. 133), pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2023 zilizofanyiwa marekebisho Mwaka 2024 kuhusu Taratibu za Afya ya Mimea na Viuatilifu.

Kwa kuzingatia hilo, Mamlaka inawataka wadau wote wa Mamlaka kuhakikisha wanafuata taratibu za kisheria zinazotakiwa, ikiwemo:-

- i. Waingizaji wa mimea na mazao wanapaswa kupata Kibali cha uingizaji wa Mimea (Plant Import Permit) kutoka TPHPA kabla ya bidhaa kuingia nchini, pamoja na kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinapita katika vituo rasmi vya mipakani kwa ajili ya ukaguzi wa afya ya mimea.
- ii. Waingizaji wa mimea na mazao wanapaswa kuhakikisha bidhaa inaambatana na Cheti cha Usafi wa Mimea (Phytosanitary Certificate) kutoka nchi husika, pamoja na kuwasilisha nyaraka zote za vibali katika Vituo vya Ukaguzi vya TPHPA.

- iii. Wasafirishaji wanatakiwa kufahamu na kuzingatia sheria na masharti ya nchi inayokusudiwa kupelekwa bidhaa, ikiwemo kuwasilisha maombi ya Cheti cha Usafi wa Mimea (Phytosanitary Certificate) pale kinapohitajika na nchi inayoagiza bidhaa.
- iv. Waingizaji wa Viuatilifu, vinyunyizi na vifaa vya unyunyiziaji wa Viuatilifu wanapaswa kupata Kibali cha uingizaji Viuatilifu au Vinyunyizi (Pesticide Import Permit or Permit to Import Pesticide Application Equipment) kutoka TPHPA kabla ya bidhaa kuingia nchini, pamoja na kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinapita katika vituo rasmi vya mipakani kwa ajili ya ukaguzi.
- v. Viuatilifu, vinyunyizi na vifaa vya unyunyiziaji vinavyopaswa kuagizwa na kuingizwa nchini ni vile tu vilivyosajiliwa kwa matumizi nchini kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Mimea.
- vi. Waingizaji na Wasafirishaji wa Viuatilifu, Vinyunyizi na vifaa vya unyunyiziaji wa Viuatilifu wanatakiwa kuambatisha nyaraka zote muhimu kwa mujibu wa Sheria, taratibu, kanuni, na miongozo ya usimamizi wa Viuatilifu nchini.

Hivyo basi, Mamlaka inatoa rai kwa wadau wote wanaojihusisha na uingizaji na usafirishaji wa mimea, mazao na Viuatilifu kuzingatia kikamilifu Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu zote zilizowekwa. Uzingatiaji huu ni muhimu katika kuzuia ueneaji wa Visumbufu vya mimea, kulinda kilimo cha Tanzania, kuhakikisha mazao ya Tanzania yanakidhi viwango vya masoko ya kimataifa, kuepusha ucheleweshaji, kuzuiliwa au kurejeshwa kwa bidhaa mipakani pamoja na usimamizi endelevu wa Viuatilifu ili kulinda afya ya walaji, wanyama na mazingira.

Imetolewa na



Prof. Joseph C. Ndunguru
MKURUGENZI MKUU

“TPHPA AFYA YA MIMEA, AFYA YA MIMEA TPHPA”